OFISI YA RAIS -TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI IGOWOLE
S.L.P 29,
MUFINDI.
TAREHE 013/12/2020

SIMU: 0755 750 973 -MKUU WA SHULE
0754 354 933 -M/MKUU WA SHULE
0754 087 454 -MTAALUMA

Kumb No 1. GSS/J.1/ADM/VOL 3/6/2021
MZAZI/MLEZI WA……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IGOWOLE WILAYA YA MUFINDI MKOA WA IRINGA KIDATO CHA KWANZA, 2021

Tunayo furaha kukuarifu kuwa mtoto wako …… mwenye namba ya mtihani ……..Amechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika Shule hii. Muhula wa kwanza Masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Hii ni Shule ya kutwa mtoto wako atarudi nyumbani kwako siku zote.
Tafadhali ieleweke kwamba mtoto wako atapokelewa kwa matumaini kuwa ateendelea na masomo yake kuanzia kidato cha **kwanza** hadi kidato cha Nne. Hatutapenda kuona mtoto anakatishwa masomo kwa sababu zisizo na msingi.

SARE YA SHULE: WASICHANA (NGUO ZA MITUMBA HAZITAKIWI)

1. Shati mbili nyeupe mikono mirefu (Tetroni)
2. Sketi mbili za marinda madogomadogo bila mikanda nyuma (rangi ya Zambarau kitambaa kizito) fundi wapo Igowole mjini. Iwe ndefu kupita magoti na ifunike soksi chini tena iwe ya heshima siyo ya kubana.
3. Soksi nyeupe ndefu (Stooking).
4. Viatu vya ngozi nyeusi tupu (bila mabaka) vya kufunga na kamba.
5. Fulana nyeupe za kuvaa ndani ya shati.
6. Sweta rangi ya bluu zinapatikana madukani.
7. Tai rangi ya zambarau kitambaa kilekile cha sare ya Shule .
8. T-Shirts zenye nembo ya Shule zinapatikana hapa Shuleni kwa bei ya Tshs.10,000/= (Model Form Six).
9. Track suit rangi ya bluu isiyo bana zipo madukani. .
10. Hijabu kwa Wanafunzi wa Kike wa Kiislam ifanane na sare ya Shule.

SARE YA SHULE WAVULANA (NGUO ZA MITUMBA HAZITAKIWI)

1. Shati mbili nyeupe mikono mirefu (Tetroni).
2. Suruali mbili za zambarau zilizoshonwa vizuri kwa heshima, mifuko miwili pembeni, mmoja nyuma isibane na ndefu kugusa kiatu na mkanda mzuri rangi nyeusi wa ngozi usiwe na chata-suruali ya kubana ni marufuku “Modal”(kubana chini ni dalili ya uhuni).
3. Viatu vya ngozi vyeusi tu (bila mabaka) vya kufunga na kamba.
4. Fulana nyeupe za kuvaa ndani ya shati.
5. Sweta la blue yanapatikana Madukani.
6. Tai rangi ya zambarau kitambaa kilekile cha sare ya Shule .
7. T-shirts zenye nembo ya Shule zinapatikana hapa Shuleni kwa bei ya Tshs.10,000/= (Model Form Six).

8. Track suit rangi nyeusi isiyo bana zinapatikana madukani.

VIFAA VINGINE KWA WOTE.

1. Picha za passport nakala 3
2. Daftari zisizopungua 15 Counter Book.
3. Lazima aje na mkebe wa vifaa vya hesabu (Mathematical set) na rula.
4. Flat spring file ni lazima kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi.
5. Dictionary ya English to English.
6. Begi jeusi la kubebea daftari la kubeba mgongoni.(school bag)
7. **NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA**

MICHEZO

1. Bukta rangi ya blue za michezo, wasichana ziwe na mpira miguuni na kuambatana na sketi fupi za kuvaa juu/Track suit rangi ya bluu (Dark blue).
2. Raba nyeusi na socks nyeusi za michezo.
3. Kwa wavulana atafutiwe sare yoyote inayofaa kwa michezo ikiwa ni pamoja na viatu vya michezo ,sare za michezo kwa maana michezo ni ajira pia.
4. Tusaidiane kuibua vipaji vya watoto wetu .

N.B Vifaa vyote vitakaguliwa

NB. Elimu ni urithi pekee mzazi unaoweza ukampa mtoto wako, mtimizie mahitaji yake kwa faida ya baadaye

FOMU ZA KURUDISHA SHULENI.
Fomu zote ziwasilishwe shuleni mara afikapo pamojaa na vifaa vyote.
Fomu A Taarifa binafsi za Mwanafunzi.
Fomu B kukubali kufuata sheria za Shule na kuthibitishwa na mzazi.
Fomu C hati ya Daktari kuthibitisha afya yake.
Fomu D Maalumu kwa Hosteli na Gharama zake zinapatikana kwa msarifu wa Shule / Mkuu wa Shule
Tunamtakia Mtoto wako afya njema na kazi nzuri yenye maendeleo na mafanikio wakati wowote wa kuwepo hapa Shuleni.

Ndimi

…..……
INNOCENT G. MGODA
MKUU WA SHULE

FOMU A

SHULE YA SEKONDARI YA IGOWOLE

TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI-HAKIKISHA MZAZI/MLEZI

TAARIFA YA MWANAFUNZI NI SAHIHI KWA MATUMIZI YA OFISI

1. Jina aliloandikishwa……
2. Majina mengine ya nyumbani……
3. Dini……
4. Tarehe ya kuzaliwa……
5. Mahalia alipozaliwa. Kijiji……..…… Kata ……..……..
   Tarafa……..Wilaya……..…
6. Jina la Baba…….
7. Jina la Mama……..…
8. Baba yuko Hai? ..... Mama yuko Hai? …….
9. Mama ana watoto wangapi? ……..
10. Wewe ni mtoto wa ngapi kwa mama?.....
11. Nyumbani unapoishi Kijiji……Kata ……..Wilaya……
    S.L.P ……..
12. Kidato ulichopokelewa…….……
13. Shule uliyotoka…….
14. Shughuli mbali na Masomo……..……
15. Kukiwa na Tatizo Taarifa ipelekwe kwa

Jina ……..
Anwani ……...
Uhusiano wenu ……..
Sahihi ya Mwanafunzi …….. Tarehe …….……...

KWA MATUMIZI YA OFISI

Namba ya kuandikishwa
Shuleni……...
Namba ya
Mtihani……
Mkuu wa
Shule……

Ndimi

……..

INNOCENT G. MGODA

MKUU WA SHULE

PICHA

FOMU B

SHULE YA SEKONDARI YA IGOWOLE
S.L.P 29, MUFINDI

YAH: KUKUBALI MASHARTI YA SHULE.

Mimi …… Niliyechaguliwa kuendelea na Masomo Kidato cha …… katika Shule ya Sekondari Igowole ninaikubali nafasi hiyo. Ninaahidi kuwa nitafuata Sheria zote za Shule zilizopo na zitakazokuja baadaye. Nitajiepusha na vitendo vyote ambavyo ni kinyume cha Sheria na taratibu za Shule. Nitakuwa mtiifu kwa Walezi wote Shuleni ambao ni Walimu na Wafanyakazi wasio Walimu.

Nitafuata maelezo nitakayopewa na Walimu na Wafanyakazi wengine wa Shule na Viongozi wote watakaokuwepo kwa mujibu wa Sheria.

Nitahudhuria vipindi vya masomo darasani na nitafanya mazoezi na mitihani yote nitakayopewa.

Ninafahamu kwamba kukiuka kwangu ahadi hii kutanipotezea nafasi yangu ya masomo.

Sahihi ya Mwanafunzi……. Tarehe……

AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi …… Mzazi/Mlezi wa ……..…….. ninaahidi nitatoa ushirikiano mkubwa kwa Walimu na Uongozi wa Shule kuhakikisha mwanafunzi mtajwa anasoma. Na nitakuwa na Desturi ya kuja mara kwa mara shuleni kujua maendeleo ya Mtoto na kuhudhuria vikao vya Wazazi (PTA) nitakapohitajika

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ……..Tarehe…….
Namba ya Simu …….

Ndimi

……
INNOCENT G. MGODA
MKUU WA SHULE

FOMU C

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

IGOWOLE SECONDARY SCHOOL

P.O. BOX 29 MUFINDI-IRINGA

To be completed by medical officer.

Students Full name ……

Age ……. Sex……..

Blood count (Red and White) ……

Stool examination ……..

Urine analysis …….

Syphilis test ……

Eye test ……

T.B test ……

Ears …….

Chest ……

Spleen ……

Abdomen ……

ADDITIONAL INFORMATION eg physical or chronical family disease,etc

……

……

I certify that the above named student is fit to pursue studies

Signature ……..

Designation ……..

Section …….

Date …….

NOTE: Medical officer at the time of examination the individual for any aliments you note.

PUPILS: You must bring this complete form when you come to school, no pupil may enroll without certificate of physical fitness.

……

INNOCENT G. MGODA

HEADMASTER

IGOWOLE SECONDARY SCHOOL
SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na 10 ya Mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila Shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Night Preparation)
d) Kuwahi katika kila Shughuli za Shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii.
f) Kutunza usafi wa Mwili mavazi na mazingira ya Shule.
g) Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote na kutunza mali ya Umma.

<u>MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE</u>

a) Wizi
b) Uasherati na Ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine, Mirungi, kubeli na kadhalika
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa Mjamzito / kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani usalam wa Shule au watu
l) Kuwa na simu ya mkononi au viambata vyake kama betri, n.k.

……
INNOCENT G. MGODA
MKUU WA SHULE